

HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFAANYIKA TAREHE 20/10/2021 UKUMBI WA MIKUTANO

MAHUDHURIO:

1. Rick Kaduri	M/Kiti
2. Paul Komba	Katibu
3. Adelina Mfikwa	Mjumbe
4. William Akili	Mjumbe
5. Majura Protas	Mjumbe
6. Hamis Kisula	Sekretarieti

AGENDA:

- 1 Kufungua kikao.
- 2 Kuridhia Agenda
- 3 Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha tarehe 26/10/2020
- 4 Kuidhinisha taratibu za manunuzi ya miradi ya maendeleo kwa njia ya force account kwa shule za Sekondari, Msingi na ujenzi wa vyoo shule za Msingi, miundo mbinu ya maji.
- 5 Kuidhinisha ununuzi wa gari aina ya Lori kusomba taka taka na shughuli nyingine za maendeleo
6. Kuridhia nyongeza ya Mkataba wa ulinzi.
7. Kuidhinisha uuzaji wa magari na piki piki chakavu.
8. Idhini ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa madarasa 51 na madarasa 8 ya shule shikizi kwa kutumia FORCE ACCOUNT na kufanya manunuzi kwa single source.
9. Taarifa ya manunuzi yaliyo fanywa kwa njia ya maandishi
10. Mengineyo
11. Kufunga kikao

MB/BZ/2021-2022/2/1 KUFUNGUA KIKAO

Katibu aliwaeleza wajumbe juu ya mabadiliko ya wajumbe yaliyo fanywa na Mkurugenzi wa Mji, ambayo amemteua Rick Kaduli kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni na Protas M. Majura aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Zabuni. Baada ya maelezo hayo alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti alifungua kikao saa 2.30 asubuhi kwa kuwashukuru wajumbe kwa kukubali kuhudhuria kikao cha kawaida cha bodi ya zabuni

HMB/BZ/2021-2022/2/2 KURIDHIA AGENDA

Ajenda zote 11 ziliridhiwa na kujadiliwa kikaoni.

HMB/BZ/2021-2022/1/3 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA TAREHE 26/10/2020

Muhtasari wa kikao cha tarehe 26/10/2020 ulisomwa na kuthibitishwa na kuwa kumbukumbu sahihi za kikao

HMB/BZ/2020-2021/2/1/4 KUIDHINISHA TARATIBU ZA MANUNUZI YA MIRADI YA MAENDELEO KUFANYIKA KWA NJIA YA FORCE ACCOUNT KATIKA NGAZI YA JAMII

Katibu wa bodi ya zabuni alikieleza kiako kuwa Halmashauri ya Mji wa Bunda inategemea kupokea fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya ujenzi wa madarasa, vyumba vya maabara shule za msingi na sekondari na ujenzi wa maboma katika zahanati Halmashauri ya Mji wa Bunda ambayo itatekelezwa kwa kutumia njia ya force account. Baada ya majadiliano wajumbe waliridhia miradi ifuatayo ifanyike kwa kutumia force account na kutekelezwa katika ngazi ya jamii kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali.

1. Ukamilishaji wa jengo la maabara shule ya Sekondari Rubana Sh. 35,000,000.00
2. Ukamilishaji wa jengo la maabara shule ya Sekondari Kunzugu Sh. 30,000,000.00
3. Ukamilishaji wa jengo la maabara shule ya Sekondari Sazira Sh. 20,000,000.00
4. Ukamilishaji wa jengo la maabara shule ya Sekondari Dr.Nchimbi Sh.40,000,000.00
5. Ukamilishaji wa darasa 2 shule ya Sekondari Rubana Sh. 22,500,000.000
6. Ukamilishaji wa darasa 2 shule ya Sekondari Kunzugu Sh. 22,500,000.000
7. Ukamilishaji wa darasa 2 shule ya Sekondari Wariku Sh. 22,500,000.000
8. Ukamilishaji wa darasa 2 shule ya Sekondari Sazira Sh. 22,500,000.000
9. Ukamilishaji wa darasa 2 shule ya Sekondari Guta Sh. 22,500,000.000
10. Ukamilishaji wa darasa 1 Shule ya Msingi Mugaja Sh.12,500,000.00
11. Ukamilishaji wa darasa 1 Shule ya Msingi Bukore Sh.12,500,000.00
12. Ukamilishaji wa darasa 1 Shule ya Msingi Bitaraguru A Sh.12,500,000.00
13. Ukamilishaji wa darasa 1 Shule ya Msingi Mcharo Sh.12,500,000.00
14. Ukamilishaji wa darasa 1 Shule ya Msingi Rwabu Sh.12,500,000.00
15. Ukamilishaji wa darasa 1 Shule ya Msingi Chiringe B Sh.12,500,000.00
16. Ukamilishaji wa darasa 1 Shule ya Msingi Kiwasi Sh.12,500,000.00
17. Ukamilishaji wa darasa 1 Shule ya Msingi Balili A Sh.12,500,000.00
18. Ukamilishaji wa darasa 1 Shule ya Msingi Butakale Sh.12,500,000.00
19. Ukamilishaji wa Zahanati ya Sazira Sh.50,000,000.00
20. Ukamilishaji wa Zahanati ya Bukore Sh. 50,000,000.00

HMB/BZ/2021-2022/2/5 KURIDHIA KUZA MALI CHAKAVU MAGARI 2 NA PIKI PIKI (BAJAJI) 2

Katibu wa Bodi aliwasilisha taarifa ya uuzaji Mali chakavu magari mawili STJ 1305 ISUZU Tipper na STJ 8075 Isuzu long Base na Bajaji mbili SM 9186 na SM 9187 pia wajumbe walielezwa kuwa mchakato wa kupata vibali cha kuuza mali hizo chakavu umekamilika kwa barua yenye Kumb Na.EG.110/474/20/106 ya tarehe 29/09/2021. Wajumbe waliridhia maombi hayo na kuelekeza taratibu ziendelee kwa mujibu wa Kanuni ya 253 ya kanuni za Fedha za Umma ,2001 (R.E 2004) kwa ajili ya kuondosha mali chakavu.

HMB/BZ/2020-2021/2/6: KURIDHIA UNUNUZI WA LORI KWA AJILI YA KUSOMBA TAKA TAKA NA SHUGHULI NYINGINE ZA MAENDELEO

Katibu wa Bodi ya zabuni aliwasilisha taarifa ya ununuzi wa gari aina ya lori tani 7 ambapo manunuzi yake yamekasimiwa kiasi cha Sh. 130,000,000.00 katika bajeti ya mwaka 2021/2022. Wakala wa ununuzi Serikalini hauna mkataba wa aina hiyo umeruhusu mchakato uendelee kupitia nukuu za bei kwa wazabuni wengine kwa barua yenye Kumn Na.CDA.260/318/06/AX/207.

Baaada ya majadiliano wajumbe waliridhia na kuruhusu mchakato uendelee kwa kufanya nukuu za bei kwa wazabuni wengine.

HMB/BZ/2020-2021/2/7: KURIDHIA NYONGEZA YA MKATABA WA ULINZI KWENYE JENGO LA HALMASHAURI, KIWANDA CHA KUFYATUA MATOFALI NA MAKAZI YA MKURUGENZI MKATABA NA. LGA/171/2020-2021/S/0S/01

Katibu wa Bodi ya zabuni aliwasilisha taarifa ya maombi ya nyongeza ya mlinzi mmoja kwenye makazi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ambapo gharama yake itakuwa kiasi cha Tsh.220,000.00 kwa mwezi hivyo kuongeza kiasi cha mkataba kutoka sh.1,820,000.00 hadi 2,040,000.00. Baaada ya majadiliano wajumbe waliridhia kuongeza mlinzi mmoja na kuelekeza taratibu zifanyike haraka ili kuimarisha ulinzi kwenye makazi.

HMB/BZ/2020-2021/2/8: KURIDHIA KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO KWA FORCE ACCOUNT NA KUFANYA MANUNUZI KWA SINGLE SOURCE

Katibu wa Bodi ya zabuni aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri imepokea kiasi cha Sh.1,020,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 51 kwa shule za Sekondari na kiasi cha Sh.160,000,000.00 kwa ya ujenzi wa shule shikizi 8. Fedha hiyo imetolewa na Serikali mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19. Baaada ya majadiliano wajumbe waliridhia taratibu ziendelee kama muongozo na maelekezo ya Serikali yanavyo elekeza.

HMB/BZ/2020-2021/2/9: TAARIFA YA MANUNUZI YALIYO FANYWA KWA NJIA YA MAAANDISHI (CIRCULAR RESOLUTION) MWEZI JULAI HADI SEPTMBA

Katibu wa Bodi ya zabuni aliwasilisha taarifa ya maamuzi ya Bodi yaliyo fanyika kwa njia ya maandishi yaani circular resolution kwa mujibu wa kanuni na. 58 ya mwaka 2013 iliyo fanyiwa marekebisho 2016. Maamuzi hayo ni ya julai 2021 hado Septemba 2021 kama ifuatavyo.

1.Ununuzi wa saruji ya kiwanda cha matofali mifuko 600 kiasi cha Sh.12,000,000.00

2.Ununuzi wa mchanga kwa ajili ya kiwanda cha matofali kiasi cha Sh.5,250,000.00

Baaada ya majadiliano wajumbe walipokea taarifa hiyo

HMB/BZ/2020-2021/2/10: MENGINEYO

Wajumbe walisisitua malipo ya posho za vikao yafanyike kwa mujibu wa sheria.


21. Ukamilishaji wa maabara Shule ya Sekondari Sazira Sh. 30,000,000.00
22. Ujenzi wa yoo vya matundu 6 shule za msingi Bunda A, Bitaraguru A, Ihale na Nya sh. 26,400,000.00
23. Ujenzi wa miundo mbinu ya maji shule za msingi Miembeni, Balili A, na Rub Sekondari sh. 35,617,140.00

HMB/BZ/2021-2022/ 2/1/11 KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao saa 4.20 asubuhi kwa kuwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao michango yao katika kikao hicho.



MWENYEKITI



TAREHE



KATIBU

